**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**TAREHE .................................**

**DODOMA**

**SHULE YA SEKONDARI MRIJO**

**S.L.P.830,**

**CHEMBA**

**Tarehe .............**

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI ………….**
**S.L.P ……………………………………..**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MRIJO HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA MKOA DODOMA MWAKA ..................**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari Mrijo mwaka ......................... na atasoma tahasusi ya (HGL/HGK)

MAHALI SHULE ILIPO NA JINSI YA KUFIKA

Shule ya sekondari Mrijo ipo katika kijiji cha Kaloleni kata ya Mrijo.

Shule ipo umbali wa Kilometa 65 Mashariki mwa Mji wa CHEMBA..Usafiri wa basi kutoka DODOMA mjini unapatikana kila siku katika kituo cha mabasi cha Machame saa 4:00 asubuhi, Nauli ni Shilingi 12,000 ni umbali wa Kilometa 170 kutoka Dodoma Mjini mpaka Mrijo.Aidha unaweza kupata usafiri wa kufika Mrijo kutoka Kondoa mjini ambapo kuna mabasi ya kutoka Kondoa kila siku saa 5 asubuhi,nauli ni sh.7,000.Unapotoka Barabara ya kutoka Arusha/Babati unashukia Kondoa Mjini,hapo kuna mabasi ya kutoka Kondoa kwenda Mrijo.Ukipanda basi lolote hakikisha unashukia **Mrijo Chini.**Hapo utapanda bodaboda kuelekea shuleni umbali wa kilometa Nne(4) kwa sh.2,000

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ...........................hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe .......................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe .........................Hakikisha unaripoti na mahitaji yote.

**2.Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i.Sketi mbili (02) au zaidi za rangi **bluu bahari** mshono wa rinda box kubwa mbele na nyuma, na mawili madogo kushoto na kulia,na Tai mbili zenye rangi ya sketi,urefu wa sketi ufike kwenye vifundo vya miguu ,kitambaa kizito cha suti.Hakuna mwanafunzi atakaye ruhusiwa kuvaa sketi fupi.Kwa wanafunzi wa Kiislamu waje na Juba mbili nyeupe ndefu zenye kufunika kifua mpaka kwenye vifundo vya mikono,na zisiwe na urembo wowote.

ii. Mashati meupe mawili (02) au zaidi ya mikono mirefu yenye mfuko mmoja. Mashati meupe ya tomato yanashauriwa zaidi.

iii.Viatu vya rangi nyeusi vya **kufunga na kamba** na visiwe na visigino virefu pamoja na soksi ndefu nyeupe jozi mbili au zaidi.Haturuhusu viatu vyenye urembo wa aina yoyote.

v. Sweta moja inayofanana na rangi ya sketi ( kuna baridi kuanzia mwezi wa sita).
vi. Track suti rangi ya bluu
vii. Sare ya kushindia (shamba dress) Gauni rangi ya kijivu na T-shirt rangi ya blue yenye nembo ya shule. (kwa anayehitaji kununua shuleni T- Shirt zinapatikana kwenye maduka yaliyokaribu na shule kwa sh.15,000. Mwanafunzi anashauriwa kuwa nazo mbili).Wanafunzi wa kiislamu waje na Juba ya Kushindia rangi ya blue
viii.Viatu vya wazi(sandals) kwaajili ya kushindia.Mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa yeboyebo.Yeboyebo zitatumika bafuni na maliwato tu.
ix. Raba nyeupe jozi moja kwaajili ya michezo pamoja na track ya blue yenye ufito mweupe na T shirt ya blue yenye ufito mweupe.

**2.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 10 makubwa na kalamu za kutosha.
ii. Nakala ya "Result slip" ya kidato cha Nne
iii. Ream (A4) bunda za Karatasi Mbili (2) kwa mwaka, uje nazo unaporipoti shuleni;
iv. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika vilivyoandaliwa na TIE pamoja na vitabu vingine.
**v.** Godoro lenye upana wa futi 2.5 au futi 3 ,**unaweza kununua godoro kwenye maduka yaliyopo karibu na shule.**
vi. Shuka mbili (02) za rangi ya bluu bahari , blanketi 1, na chandarua 1;
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko
x. Jembe lenye mpini na Ndoo kubwa ya lita 20,na ufagio mmoja wa chelewa kwaajili ya usafi wa nje na mwingine wa kusugulia ndani (hard bloom) wenye mpini mrefu kwa wanafunzi wa **HGL**.
xi. Panga,na ndoo kubwa ya lita 20 ,Squeezer(mpira wa kukaushia maji), na mfagio laini (soft bloom) yenye mpini mrefu kwa wanafunzi wa **HGK**
xii. Kitambulisho cha BIMA ya Afya cha NHIF kwaajili ya matibabu.
xiii. Sanduku(tranker) la kutunzia vifaa vyake.
xiv. Majalada (files) mawili kwaajili ya kutunzia nyaraka zake ofisini na kazi zake za darasani. Unashauriwa kuwa na majalada ya nailoni au plastiki.

**1.1 Michango mbalimbali**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango hii ilipwe kwenye akaunti ya shule,Mrijo Secondary School A/C Na. 50201200103 NMB. Mwanafunzi aje na Risiti ya Bank siku ya kuripoti. Michango ya cash haitapokelewa.**

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kufanya mitihani yote kwa mujibu wa ratiba
v. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
vi. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule.
vii. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule; mwanafunzi haruhusiwi kusuka na kufuga nywele ndefu.
viii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
ix. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
x. Kutunza mali za shule;
xi. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xii. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule kwasababu maalum**.

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kusuka nywele.Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu.
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara au bangi.
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira yoyote ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xviii. Kutoka kwenye mipaka ya shule bila kibali.

**3.Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE TAFADHALI, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0789607312/ 0755638312 Mwl.HANCE F.MWAITETE**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0784890940 (Mwl.MARVIN G. NKUBA)**
- **Mwandamizi Taaluma ; 0686020623 (Mwl.HAJI I.MUSSA)**
- **Mwandamizi Nidhamu: 0719528188 (Mwl.WEMAELI K. ADILI )**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MRIJO**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………**
**Jina la Mkuu wa Shule :HANCE F. MWAITETE**
**Mhuri wa Mkuu wa Shule ……………………….**

**FomuNa. 1AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi____________________________wa S.L.P_Mji____________________Simu _________________na mwenye picha hapo juu. Ambaye kazi yangu ni __________________natamka hapa kama mzazi/mlezi wa_ __________________.Ninakubali kwa hiari yangu mwanangu asome katika Shule ya Sekondari Soya kuanzia tarehe_____________.Ninaahidi kamaifuatavyo:-

1. Kwamba nimekubali chaguo alilopewa mwanangu na sitamruhusu kubadilisha hadi apate kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika.
2. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote kama vilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga ikiwemo SARE KAMILI ya shule bila kuharibu chochote.
3. Ninatambua yakuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu elimu na nitashirikiana nao bega kwa bega kwa masuala ya nayomuhusu mwanangu kitaaluma na nidhamu ili aweze kufikia malengo yake na ya Taifa.
4. Naahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoainishwa katika fomu hii achukuliwe hatua stahili za kinidhamu kama ilivyoorodheshewa.

Jina:__________________________________ saini______________________

Tarehe:___________________Uhusiano na mwanafunzi:____________________

**<u>FomuNa.2</u>  AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi mwanafunzi____________________________________________Wa kidato cha Tano chaguo __________________________(tahasusi) mwaka wa masomo 2025/2026.Ninakiri kusoma,kuelewa na kuahidi kutii taratibu zote zilizoainishwa katila fomu iliyotumwa kwangu na Mkuu wa shule ya Sekondari Mrijo. Nitatoa ushirikiano wa kutosha kwa walimu wangu na shule kwa ujumla katika muda wangu wote nitakao kuwa shuleni ili niweze kupata elimu na kuendeleza jamii na Taifa langu.

Jina:________________________________________________ Saini____________________

Tarehe:__________________________________________________________

**FomuNa.3**

**KIAPO CHA MZAZI/MLEZI**

Mimi:__________________________wa S.L.P______________Mji_____________

Na________________. Nakiri kukaa na kuzungumza na mwanangu juu ya taratibu nasheria za shule na ninaahidi kumsaidia na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Mkuuwa Shule na walimu kwa muda wote ambao mwanangu atakapokuwa katika shulehii. Ninatambua madhara ya mwanangu kutembelewa na wageni wasioeleweka wakati akiwa shuleni na ninaomba shule iwatambue watu watatu(3)ambao wanahusika katika muda wote ambao atakuwa shuleni nao ni:-(ambatanisha picha passport size zao)

*Picha ya ndugu wa Kwanza*

Jina:_______________________________________ Kazi:__________________ Makazi:

______________________ Simu:_________________________________

Uhusiano na mwanafunzi:_________________________________________________

*Picha ya ndugu wa Pili*

Jina:_________________________________________________________ Kazi:___________

Makazi:________________________ Simu:____________________

Uhusiano na mwanafunzi:__________________________________________________________

*Picha ya ndugu waTatu*

Jina:_______________________________________ Kazi:__________________ Makazi:

Simu:________________________________
______________________
Uhusiano na mwanafunzi:________________________________________________

**Fomu Na. 4**

MRIJO SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 830
CHEMBA

**MEDICAL EXAMINATIONFORM**

Tobe completed by Medical Officer from a known Public Hospital or Health Centre in respect to all entrants

Full name……………………...…………..Age……...Sex…………year…....

1.Blood count(RedandWhite)……………………………………...
2.Urinal analysis Test……………………………………………….
3.Syphilist est…………………………………………………
4.T.B.……………………………………………………………
5.EyeTest……………………………………………………
6.Ears……………………………………………………………
7.Spleen…………………………………………………………
8.Abdomen……………………………………………………….

ADDITIONAL INFORMATION:e.g.Physical impairment,family disease,chronic infections etc.

………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………

I certify tha tthe above named individual is fit to pursue studies as stated above

|  |  |
|---|---|
| ……………………………….. | ……………………………… |
| Name and Designation | Signature and Official stamp |

……………..……….………STATION DATE

**NOTE:**

1. Medical officer during the course of this Examination please attend the individual according to any diagnosed case.
2. The dully filled form must be handed to the Head of the School during registration week,under No circumstances should a student be registered without certification of his/her physical fitness.